

Maswali

1. Musa alikua wapi?
2. Mmisri alikuwa anamfanyaje Mwisraeli?
3. Musa alimfanyaje Mmsri?
4. Waisraeli wawili walikuwa wanafanya nini?
5. Waisraeli wawili waliambiaje Musa?
6. Musa alienda wapi?
7. Musa aliona nini jangwani?
8. Mungu alimwambia Musa afanye nini?
9. Mungu alimwambia Musa aende wapi?
10. Mungu alimwambia Musa aseme nini kwa Farao?

Majibu

1. Musa alikua kwa jumba la Mfalme.
2. Mmisri alikuwa anampiga Muisraeli.
3. Musa aliua Mmisri.
4. Waisraeli wawili walikuwa wanapigana.
5. Waisraeli wawili walisema, "Utatuua sisi vile uliua Mmsri?"
6. Musa alienda Midiani.
7. Musa aliona kichaka kinawaka moto.
8. Mungu alimwambia Musa atoe viatu kwa sababu mahali hapo palikuwa patakatifu
9. Mungu alimwambia Musa aende kwa Farao.
10. Mungu alimwambia Musa aambie Farao aachilie watu wake waende

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

15 Kichaka (kijiti) kinawaka moto

Marejeo

Kutoka 3

Kiini cha somo

Kuonyesha ukuu wa Mungu na ni lazima aheshimiwe

Maneno maalum

- 1 Jumba la mfalme Farao + Musa anatembelea watu wake + Mmisri anampiga Mwisraeli + Musa anaua
- 2 Waisraeli wanapigana + Mwana wa mfalme +Musa anaogopa
- 3 Musa anatoroka + Midiani + kichaka chawaka moto + Mungu anazungumza + toa viatu + mahali patakatifu
- 4 Watu watoka Misri + tauni + Musa anarudi Misri

15.1 Musa alikuwa katika jumba la mfalme Farao kama mwana wa bintiye. Siku moja, alienda kuona watu wake. Aligadhabika sana kwa kuona vile wanatezwa na wasimamizi.

Aliona Mmisri anapiga Mwisraeli, na akakasirika. Akaangalia huku na huku na alipoona hakuna mtu amemuona, akamuua Mmisri na kumficha ndani ya mchanga.

15.2 Siku ifwatayo, akaenda tena kuona watu wake. Waisraeli wawili walikuwa wanapigana, "Mbona mnapigana?" aliwauliza.

"Nani alikufanya mtawala na mwamuzi wetu?" Waisraeli walimuuliza. "Unataka kutuua vile uliua Mmisri jana." Musa aliogopa sana alipojua kwamba walimuona akiua Mmisri.

15.3 Musa akatoroka akaenda nchi ya Midiani. Akamuoa binti wa kuhani wa Midiani. Aliishi jangwani akichunga kondoo.

Siku moja, alikuwa anachunga kondoo akaona kichaka kinawaka moto. Kichaka kiliwaka na kuwaka lakini hakikuungua. Musa akasema, "Nitaenda niangalie maajabu ya kufanya kichaka kisiungue."



Sauti ya Mungu ikatoka kwa hicho kichaka ikiiita Musa. "Musa! Musa!" Mungu aliita. "Mimi hapa," Musa akasema.

Mungu akamwambia Musa, "Usikaribie hapa, toa viatu vyako, kwa sababu pahali umesimama ni mahali patakatifu."

Mungu alimwambia Musa kwamba ameona vile Wamisri walikuwa wakiteza watu wake. Alikuwa amesikia kilio chao. Kwa ajili ya wasimamizi wabaya.

15.4 "Nitakutuma kwa Farao ill uwachukue watu wangu, wana Waisraeli watoke Misri," Mungu alimwambia Musa.

Musa akasema, "Mimi si wa maana sana kwenda kwa Farao na niwaongoze Waisraeli watoke Misri"

Mungu akamwambia, "Nitakuwa na wewe. Utamwambia Farao kwamba Bwana Mungu amekutuma na lazima uwaache waende wamtotee Mungu dhabihu. Farao hatawaachilia muende lakini nitanyosha mkono wangu niwapige na tauni halafu Farao atamuacha muende."



